

## Maswali

1. Wakubwa wa dini walinuia kufanya nini?
2. Mwanafunzi yupi alienda kwa Wakuu wa Makuhani na kwa nini?
3. Mbona alifanya hivyo?
4. Yuda alijuaje wakati mzuri wa kumsaliti Yesu?
5. Yesu alisema wakati gani kwamba mmoja wa wanafunzi wake anaenda kumsaliti?
6. Baada ya chakula cha Pasaka Yesu alienda pahali patulivu, alifanya nini?
7. Yesu aliporudi kulikokuwa wanafunzi, walikuwa wanafanya nini?
8. Yesu aliona nani akija alikokuwa, na nani?
9. Yuda alipeana ishara gani kuonyesha walinzi kwamba Yesu ndiye walimtaka?
10. Yesu alikubali kukamatwa namna gani?

## Majibu

1. Walikuwa wanatafuta namna ya kumkamata Yesu.
2. Yuda alienda kwa Wakuu wa Makuhani kumsaliti Yesu.
3. Alitaka pesa.
4. Wakati Yesu alienda pahali patulivu ili apumzike.
5. Wakati alikuwa na wanafunzi wake kwa chakula cha Pasaka.
6. Aliambia baadhi ya wanafunzi wake kukesha hali anaomba.
7. Wanafunzi walikuwa wakilala
8. Yesu aliona Yuda akija na watu waliobeba silaha na tochi.
9. Kama ishara, Yuda alimbusu Yesu kuonyesha ndiye walimtaka.
10. Yesu alikubali kukamatwa bila mabishano akijua haya yote yalikuwa mapenzi ya Mungu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 44 Yuda anasaliti Yesu

## Marejeo

Marko 14:1-2, 10-11, 19-21, 32-46

## Kiini cha somo


Kuonyesha ujasiri mkuu wa Yesu na vile alikubali mapenzi ya Mungu. Yesu alituonyesha vile tunaweza kujali rafiki wetu na mwenendo wetu kwa adui. Tunapaswa kufuata mfano wake katika maisha yetu.

## Maneno maalum

1. Wakuu wa Makuhani + haja + kamata Yesu + sababisha ghasia + msongamano
2. Yuda + mpango wa kusaliti + pesa
3. Yuda + makuhani + pesa + wakati wa utulivu
4. Pasaka + Yesu + bashiri kusalitiwa + jogoo awika
5. Bustani + Yesu anaomba + wanafunzi wanalala.
6. Tochi + zinamlika + sauti + Yuda + busu + Yuda + kamata
7. Yesu + kutimiza amani + mapenzi ya Baba

**44.1** Siku ya Pasaka ilikuwa inakaribia na wakuu wa Makuhani walikuwa wanatafuta nafasi ya kumkamata Yesu. Lakini waliogopa kwamba watu wangepanya ghasia kwa vile Yesu alikuwa amekubaliwa na wengi na wangepinga. Kwa juma moja wasimamizi wa dini waliuliza Yesu maswali ili wampate na makosa na wamshike. Waliona alikuwa ananyemelea mamlaka yao.

**44.2** Yuda, mmoja wa wanafunzi thenashara alienda kwa wakuu wa Makuhani kumsaliti Yesu. Walifurahi kusikia hayo na wakaahidi kumpea pesa. Hatujui sababu zilizomfanya Yuda amsaliti Yesu, lakini alikuwa mtu aliyependa pesa sana. Tuelewe ya kwamba Yesu alisalitiwa na mmoja wa wanafunzi wake kwa malipo ya pesa.



**44.3** Yuda alienda Yerusalemu na akasikizana na Makuhani juu ya pesa atakazolipwa na vile atawaongoza mpaka pahali Yesu alikokuwa akipumzika inje ya mji. Hapo pahali palikuwa patulivu na ni penye Yesu alikuwa ameenda kukula chakula Pasaka na rafiki zake.

**44.4** Yesu alishikilia sherehe hii kuwa na maana kuu. Jioni hiyo, wakati walikuwa wamekaa wanakula hiyo Pasaka, Yesu alisema, "Amini nawambia ukweli, mmoja wenu atanisaliti – anayekula pamoja nami." Walihuzunika na kuuliza mmoja baada ya mwingine, "Kweli sio mimi?" Yesu aliwajibu, "Ni mmoja wa ninyi thenashara, ambaye anachovya mkate kwa bakuli pamoja nami." Petro alimwambia, "Sitakuacha uende. Yesu alimwambia, "Kabla jogoo iwike, utasema mara tatu kwamba haunijui." Kabla wamalize kukula, Yuda aliamka na kuenda.

**44.5** Baada ya chakula walienda wote pahali walikokuwa wanapenda kuenda (Yuda alifahamu hapo pahali na alijua watakawia pale). Yesu alichukuwa Petro, Yakobo na Johana. Walienda mbeli chini ya miti na wengine walibaki karibu na lango. Aliwambia, "Kesheni." Alisonga mbele kidogo katika bustani na akaomba. Alijua anaenda kufa.

**44.6** Aliporudi walikokuwa wanafunzi wake, aliwakuta wanalala. Akawambia, "Bado mnalala-huu ndio wakati mwana wa Adamu anasalitiwa. Msaliti ndiyo huyu anakuja." Kulikuwa na sauti za watu na mwangaza wa tochi ukimlika mlika. Yuda alikuwa amekuja na kikundi cha watu waliokuwa na silaha kumkamata Yesu. Yuda alikuwa amewambia, "Mtu nitakaye mbusu ndiye huyo mnamtaka." Alienda mpaka kwa Yesu na akambusu. Mlinzi aliyekuwa na silaha alichukuwa Yesu na kwenda naye.



**44.7** Yesu alikuwa na upweke na uchungu sana kwa sababu wanafunzi na marafiki wake walikuwa wanalala. Yuda hakukuwa na moyo mzuri, alitumia ishara kumsaliti Yesu kwa maadui wake. Yesu alikuwa mtulivu na alikubali kushikwa bila kushindana akijua hiyo ilikuwa mapenzi ya Mungu.